# AAP N° 42

# SWAHILI FORUM II

Edited by Rose-Marie Beck, Thomas Geider, Werner Graebner



JUNI 1995

SWAHILI FORUM II

Edited by

Rose-Marie Beck

Thomas Geider

Werner Graebner

Afrikanistische Arbeitspapiere
Institut für Afrikanistik
Universität zu Köln
50923 Köln
Germany

Cover design. Donald A. Lessau / R.-M. Beck / Th. Geider

© by the editors

ISSN O178-725X

*AAP 42 (1995): 158-167*

# SENTENSI ZA KUONYESHA MATUKIO YANAYOTOKEA KWA PAMOJA

THILO C. SCHADEBERG

Kiswahili has many ways to express different relations that may hold between two events occurring at the same time. In this paper I examine and contrast the meanings of two types of verbal forms: those with the class 16 relative concord marker *-po-* and those with the tense marker *-ki-*. All examples are taken from a single small novel. I conclude that forms with PO tell us *where* or, more frequently, *when* something else occurred, whereas events presented in the KI-tense describe the situation existing at the time of some other event ("situative"). When that other event is non-factual the situation presented in the KI-tense expresses a condition. Elsewhere, the situation presented in the KI-tense may be backgrounded (in the discourse analysis sense of the term), but it may also be the main event that is hidden behind a more superficial situation (*pace* Contini-Morava 1989).

## 1. Utangulizi

Lugha ya Kiswahili inatumia njia mbalimbali kueleza kwamba matukio mawili yanatokea kwa pamoja. Angalia methali hii:

(1) *Kutwanga nisile unga, nazuia mchi wangu.*
When I pound without eating from the flour, I stop my pestle.

Kitenzi cha kwanza, *kutwanga,* kina umbo la jina kitenzi. Kitenzi cha pili, *nisile (unga),* kinatokea katika hali ya matakwa ya kukanusha. Kitenzi cha tatu, *nazuia (mchi wangu),* kinatokea katika hali ya wakati uliopo (au: hali ya wakati wa kawaida). Basi, tukisikia methali hii, kwa namna fulani tunafahamu kwamba matukio hayo matatu ya kutwanga, ya kutokula na ya kuzuia yanatokea kwa pamoja, wakati ule ule.

Katika makala haya napenda kujadili maumbo ya aina mbili ya vitenzi ambayo hutumika hasa kwa kuonyesha kwamba matukio yanatokea kwa pamoja: maumbo yenye PO na hali ya KI. Ushahidi wangu wote unatoka riwaya moja tu, *Matatu ya Thamani,* iliyotungwa na Salim A. Kibao (Nairobi: Heinemann, 1975.) Kijitabu hiki kimetaipiwa kwa kompyuta na kundi la wanafunzi pamoja na mimi, na halafu nilitumia programu ya kuainisha kimofolojia AINI (Schadeberg na Elias, 1989) kwa kutafuta mifano yote inayohusika na mada yangu.

## 2. Vitenzi vyenye PO

Tukiangalia vitenzi vyenye PO peke yao, inaonekana kwamba si taabu kubwa kufahamu maana ya kiambishi hicho.

Kiambishi-rejeshi *-po-* ni alama ya kuonyesha upatanisho na ngeli 16. Ngeli hii hasa ni ngeli ya mahali, lakini kitenzi chenye kiambishi-rejeshi *-po-* kinaweza kurejea kwa kitangulizi ambacho ni ama mahali ama wakati. Mara nyingi kitangulizi hakitajwi kiwe neno katika mazingira. Riwaya yetu inatoa mifano 125 ya *-po-;* miongoni mwao mifano 5 tu inarejea kwa mahali na mifano 120 inarejea kwa wakati.

(2) *akapaonyesha alipomkuta* (UK 42)
he indicated [the place] WHERE he had found it [the horse]

(3) *Basi Sudi akafika alipokuwa yule jambazi.* (UK 21)
And then Sudi arrived [at the place] WHERE that crook was.

(4) *jana uliponipa ile barua* (UK 46)
yesterday WHEN you gave me that letter

(5) *Walipofika mjini, ...* (UK 19)
WHEN they arrived in town, ...

Kiambishi *-po-*, kama viambishi-rejeshi vyote katika lugha ya Kiswahili, kinaweza kutokea pamoja na viambishi vya hali *-na-*, *-taka-*, *-li-* na *-si-*. Kwa sababu hii, napinga matumizi ya istilahi "hali ya *-sipo-*". Hapana "hali ya *-sipo-*" isivyo "hali ya *-takavyo-*". (Zipo aina mbili nyingine za kutunga sentensi za urejeshaji katika Kiswahili. Aina hizo hazitumiki mara nyingi kwa maana ya kiwakati ambayo inatuhusu hapa; kwa hiyo hatuziangalii katika muhadhara huu.)

Katika riwaya yetu mifano ya hali nne za urejeshaji inayotumika pamoja na *-po-* yenye maana ya kiwakati inagawanyika kama ufuatavyo:

(A) Kugawanya kwa PO yenye maana ya kiwakati:

| | | |
|---|---|---|
| *-li-po-* | wakati uliopita | 109 |
| *-na-po-* | wakati uliopo | 6 |
| *-taka-po-* | wakati ujao | 4 |
| *-si-po-* | hali ya kukanusha | 1 |
| jumla | | 120 |

**3. Hali ya KI**

Tukitafsiri vitenzi vyenye kiambishi cha hali *-ki-* inaonekana kwamba hali hii inaweza kuleta ujumbe zaidi ya mmoja. Vitabu vya kuwafundisha wageni hutia mkazo kwa kutofautisha matumizo ya "hali ya kutokea kwa pamoja" na ya "hali ya sharti". Mfano wa aina hii ni sarufi ya Ashton (1944:138):

(6) Ashton 1944, UK 138:

The *-ki-* tense, as a simple tense, corresponds to two totally different forms in English:

(i) A Present Participle, when that participle refers to an imcomplete action.

*Tuliwaona watoto wakicheza.* We saw the children playing. ...

(ii) A conditional clause, when used without reference to any definite time. ...

*Ukimwona Hamisi, mwambie namtaka.* If you should see (lit. you-him-seeing) Hamisi, tell him I want him.

Hata hivyo, wataalamu wa isimu wengi wanakubali kwamba hali hii ina MAANA moja ambayo ni msingi wa UJUMBE unavyotokea kwa namna mbalimbali katika matumizi yake. Tusikilize maelezo ya Delius & Roehl (1939:68) juu ya hali hii:

(7) Delius & Roehl 1939, UK 68:

Die Zeitsilbe *-ki-* bezeichnet eine Nebenhandlung, die während der Haupthandlung noch andauert, oder die sie bedingt, oft auch einen Zustand. Die mit der Zeitsilbe *-ki-* gebildeten Formen können oft durch das deutsche Mittelwort (Participium) oder durch die Bindewörter (Konjunktionen) "wenn, indem, als, während" umschrieben werden.

Kiambishi cha wakati *-ki-* kinaeleza habari saidizi inayodumu wakati wa habari kuu, au ambayo ni sharti ya habari kuu, na mara nyingi ni hali. Vitenzi vyenye kiambishi cha wakati *-ki-* vinatafsiriwa kwa Kijerumani kwa ...

Dammann (1956) amependekeza kuita hali ya KI kwa istilahi ya "Situativ", yaani hali ilivyo, nami nitafuata pendekezo hili.

Kwa kweli, matumizi mawili anayoyataja Ashton hayatoshi. Anavyoeleza Contini-Morava (1989:130) yapo matumizi ya tatu, ambayo ni matumizi huru yasiyotegemeana na sentensi nyingine kwa namna ya kisintaksia.

(8) *Lakini alikuwa hana la kufanya, na haikuwa kosa la mtu mwingine bali akijilaumu mwenyewe.* (UK 5)
But there was nothing he could do, and it was not anyone else's fault, on the contrary, HE HAD ONLY HIMSELF TO BLAME.

(9) *Akisema tu, kwani haja yake ilikuwa kumfitini ili afikiwe na madhara.* (UK 32)
SHE WAS JUST TALKING, since her intention was to cause him trouble so that he would come to harm.

### 4. Matumizi ya hali ya KI

Katika riwaya yetu kuna mifano 100 ya hali ya KI (bila kuhesabu marudio na bila kuhesabu tungo zenye kitenzi kisaidizi *kuwa,* kwa mfano *alikuwa akipata shilingi mia mbili na hamsini;* UK 2.) Matumizi matatu yamegawanyika kama ifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| (B) | Matumizi ya hali ya KI: | huru | 12 |
| | | wakati mmoja | 24 |
| | | masharti | 64 |
| | | jumla: | 100 |

Ujumbe wa hali ya KI unategemea sana hali ya muktadha unaohusika. Muktadha ukiwa hadithi kwa jumla au sentensi inayoeleza jambo lililotokea, ujumbe wa hali ya KI huwa ni mambo yanayotokea pamoja. Lakini kama muktadha unaohusika ni sentensi ya kueleza jambo linalowezekana lakini halikutokea au bado halijatokea, basi ujumbe wa hali ya KI unafanana na sharti.

- Vitenzi vinavyoleta ujumbe wa wakati mmoja hutokea pamoja na vitenzi katika hali mbalimbali yanayoeleza matukio ya wakati uliopita, yenye alama za *-li-*, *ha- -ku-* na *-ka-* (taz. mifano 10–11). Vitenzi vinavyoleta ujumbe wa masharti hutokea pamoja na vitenzi katika hali mbalimbali nyingine, kama vile: hali ya amri, hali ya matakwa, hali ya wakati ujao, na pia pamoja na kiarifu bila kitenzi — na kila moja inaweza kutumiwa katika hali ya kukanusha (taz. mifano 12–14).

(10) *Alipofika ndani, hakuwa na haraka ya kumwita mkewe akijua atachekwa.* (UK 40)
When he came in he was in no rush to call his wife, knowing that he would be laughed at. [hali ya wakati uliopita ya kukanusha]

(11) *mara wakaingia askari wakimtafuta aliyeiandika barua ile* (UK 25)
suddenly soldiers entered in search for the one who had written that letter
[hali ya kufuatana]

(12) *Ukitumwa tumika. Ukiaminiwa jiaminishe. Ukiona la ajabu liangalie.* (UK 22)
If you are sent on an errand, let you be sent. If you are trusted, be trustworthy. If you see anything special, take a good look. [hali ya amri]

(13) *na pengine akitaka aende akamwone* (UK 52)
and maybe, if he wished, he might go and look at her [hali ya matakwa]

(14) *Ama kweli hapa nikishindwa, basi ni uzembe wangu.* (UK 10)
It is really true: if I fail here, it is my own laziness.
[kiarifu cha kijina, bila kitenzi]

Tufahamu vizuri kwamba ujumbe wa hali ya KI hautegemei hali ya kitenzi fulani mazingirani, kama ni wakati ujao au wakati uliopita, bali unategemea ujumbe wa kitenzi hicho ambao ama ni matukio ya kweli ama ni matukio yasiyotekelezwa. Jambo hilo linafahamika wazi tukiangalia mifano yenye vitenzi katika hali ya NA au ME au hali nyingine ambazo zinaweza kuhusika nyakati mbalimbali.

(15) *Na Sudi alikuwa ametulia anawaangalia nduguze kwa makini sana, humo moyoni mwake akisema, "Mlinidhulumu, mkanifukuza, lakini Mungu hakunitupa ..."* (UK 58)
And Sudi quietly looked at his brothers with great serenity, saying by himself: "You have done me injustice, you have chased me away, but God did not forseake me ..."

(16) *Akiingia chumba hiki hataki kutoka, akiingia chumba kile ni vivyo hivyo.* (UK 26)
When he entered one room he did not want to leave, and when he entered another one, it was the same.

(17) *nikichelewa naweza kwenda kuadhibiwa na Mfalme* (UK 37)
if I am late I could be punished by the King

Katika mfano (17) kuna vitenzi visaidizi viwili. Cha kwanza, *naweza,* kinaeleza kwamba adhabu ni uwezekano, si hakika, na cha pili, *kwenda,* kinaeleza kwamba uwezekano huo ni kitu cha wakati ujao. Kwa hiyo tunafahamu kwamba ujumbe wa kitenzi chenye hali ya KI ni kama sharti. — Mwisho wa sehemu hii tuangalie mfano mwingine:

(18) *ukimuuliza kitu hata kama unamuuliza kwa uzuri atakujibu kwa ufedhuli* (UK 31)
if you ask him something, even if you ask him nicely, he will answer you rudely

Ni dhahiri kwamba maana ya *ukimuuliza* na maana ya *kama unamuuliza* karibu ni moja. Lakini ninavyoona iko tofauti ndogo. Kitenzi chenye hali ya KI kinahusu kila tukio la swali lolote, yaani yanaeleza hali ilivyo kwa ujumla, bali kishazi *kama unamuuliza kwa uzuri* kinahusu sehemu tu ya maswali yanayoweza kuulizwa.

**5. Ulinganisho wa KI na PO**

Sasa tumefika mahali ambapo inatubidi kutofautisha maana ya hali ya KI na ya maumbo yenye *-po-*. Yote mawili yanaeleza kwamba matukio mawili yanatokea kwa pamoja. Tukitafsiri *akija* na *anapokuja* kwa Kiingereza au kwa Kijerumani, mara nyingi tunashindwa kuonyesha tofauti na kutafsiri kwa namna moja: *when he comes / wenn sie kommt.* Tofauti ya kisemantiki baina ya maumbo hayo lazima yafuatane na maana zao mbalimbali. Tofauti ni hii: Kitenzi cha hali ya Ki kinaeleza HALI ILIVYO wakati wa matukio mengine, kitenzi cha umbo lenye *-po-* kinaeleza LINI tukio lingine linatokea.

Tofauti hii inasababisha kwamba kila hali au umbo linapendelea kujiunga na kundi la vitenzi la pekee. Vitenzi vinavyoeleza matukio yanayodumu kwa muda fulani hufaa zaidi kuunganishwa na hali ya KI; vitenzi vinavyoeleza matukio ya kitambo hufaa zaidi kuunganishwa na vitenzi vyenye maumbo yenye *-po-*. Orodha C inaonyesha vitenzi ambavyo vinatokea zaidi ya mara mbili kwa maumbo yenye *-po-*.

(C) Vitenzi vinavyopendelea *-po-:*

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| *-fika* | arrive | 33 | *-rudi* | return | 4 |
| *-cha* | dawn | 11 | *-uliz(w)a* | (be) ask(ed) | 4 |
| *-ona* | see | 7 | *-amua* | decide | 3 |
| *-ondoka* | go away | 6 | *-isha* | finish | 3 |
| | | | *-ja* | come | 3 |
| | | | *-sikia* | hear | 3 |
| | | | *-toka* | leave | 3 |

Vitenzi hivi kumi na kimoja ni theluthi mbili za mifano yote 120, na vitenzi vine vya kwanza karibu ni nusu. Vitenzi hivi vyote vinafaa zaidi kueleza mambo yanayotokea kwa kitambo; kitenzi *kucha* hutumika kama *kulipokucha,* yaani 'siku nyingine'. Kwa hiyo, vitenzi hivi vinafaa kueleza barabara wakati tukio jingine linapotokea.

Kwa upande mwingine, vitenzi 34 kwa hali ya KI vinavyoeleza matukio kwa pamoja, vingi vyao hurejeshea matukio yanayodumu. Vitenzi viwili tu vinatumika zaidi ya mara mbili

(yaani, mara nne): *kuwa* na *kuitwa*. Matumizi haya ya *kuitwa* ni ya kuvutia: Mifano mine yote ni "huru", yaani hayategemei sentensi nyingine, tena inatoa habari mpya katika hadithi.

(19) *Sudi akamuuliza, "Sasa jina lake akiitwa nani mbona hujalisema? Umeeleza tu. Tafadhali niambie jina lake". ... Hamu akasema, "Jina lake akiitwa Sudi".* (UK 58)
Sudi asked him: "Now what is his name, you have not yet told it. You have just told the story. Please tell me his name." ... Hamu said: "His name is Sudi".

Ikiwa ni kweli kwamba hali ya KI maana yake ni kueleza hali ilivyo wakati wa matukio mengine, wapi ni habari kuu? Ninapendekeza kwamba habari kuu ni sentensi ya kinomino *jina lake (ni) fulani.*

Kuna vitenzi viwili vinavyotokea kwa hali ya KI na kuwako kwenye orodha C ya vitenzi vinavyopendelea *-po-* vilevile. Ingefaa kuangalia mifano:

(20) *Sudi alipowaona tu, aliwatambua kuwa ni kaka zake.* (UK 56)
When Sudi saw them, he immediately recognized them as his elder brothers.

*Akiona atakaa maisha yake yote pale.* (UK 6)
He felt he would stay here for the rest of his life.

(21) *na nikawa nafanya kazi kama kawaida mpaka uliporudi.* (UK 46)
and I went about my duties as normal until you returned.

*hawakumwona akirudi na hawakujua alikokwenda.* (UK 40)
they had not seen her return and did not know where she had gone.

Kila mara kishazi chenye *-po-* kinaeleza wakati kamili wa tukio jingine, bali kishazi kwa hali ya KI kinaeleza hali ilivyo wakati wa tukio jingine.

Mifano yenye *-na-po-* si mingi lakini inafanana sana kisemantiki na mifano ya hali ya KI. Tuangalieni sentensi zifuatazo:

(22) *Kila anapokumbuka mambo yaliyompata jana usiku mwili unamsisimka.* (UK 29)
Each time he remembered what had happened to him the night before, he got gooseflesh.

*Kila akikaa Sudi alikumbuka maneno yake aliyoyanunua kwa shilingi mia tatu.* (UK 33)
Whenever he paused to think Sudi remembered his three words which he had bought for three hundred shilling.

Ninapendekeza kwamba ipo tofauti ndogo ya kisemantiki: kishazi chenye *-na-po-* kinarejea kwa kila tukio moja kwa moja, bali kishazi cha hali ya KI kinarejea kwa matukio yote kwa ujumla. (Tofauti hii inafanana na tofauti baina *each* and *every* kwa Kiingereza.)

Vitenzi vyenye *-taka-po-* vinaeleza wakati kamili wa tukio jingine lijalo, bali vitenzi vya hali ya KI havirejeshei wakati wowote peke yao ila vinaweza kujiunga na sentensi nyingine ya wakati ujao.

(23) *Basi alitia azma akasema, "Mungu atakaponipa mwana, nitafanya juu chini nimsomeshe kwa kadiri ya uwezo wangu."* (UK 13)

And he made a resolution and said: "If God gives me a child, I shall do my utmost best to give him an education."

*Mungu akipenda, mtaondoka katika shida mliyo nayo.* (UK 58)
God willing, you shall get out of your present troubles.

Mwisho wa sehemu hii, siwezi kuruka mfano mmoja ambao unaelekea kutofuata uchambuzi wangu.

(24) *Basi ndiye atakayekuwa badala yangu, iliyobaki ni siku ya kumtawaza na hii mtaarifiwa ikifika.* (UK 50)
So he is the one that shall be my successor, which leaves only the day of his coronation to be settled, and of this you shall be informed when it comes.

Katika sentensi hii hali ya KI inatokea pamoja na kitenzi *kufika* ambacho hasa ni kitenzi cha kupendelea *-po-* kwa sababu hueleza tukio la kitambo. Tena, inarejea kwa kishazi kingine cha wakati ujao ambayo kwa kawaida ni alama ya ujumbe wa sharti. Kwa nini mwandishi ametumia hali ya KI badala ya *-taka-po-*? Napendekeza maelezo hayo: Maneno haya ni maneno ya mfalme ambayo anayataja kwa kufunga mkutano wa kutangaza nani atakuwa mfalme baada yake. Lakini maneno ya mwisho kuhusu siku, *hii mtaarifiwa ikifika,* si maelezo juu ya wakati kamili, bali mfalme anaeleza kwamba bado hana nia ya kutangaza siku yenyewe, *(siku) ikifika* si siku kamili lakini ni muda mrefu zaidi siku itakapokaribia.

**6. Utaratibu wa habari: yaliyo mbele na yaliyo nyuma**

Kila habari ina utaratibu wake. Tunaweza kugawanya habari kwa matabaka au viwango viwili. Kiwango kimoja ni habari kuu, yaani mfululizo wa matukio katika hadithi, au mstari wa hadithi, au mambo yaliyo mbele ili tuweze kuyaangalia vizuri. Kiwango kingine ni habari-saidizi, yaani maelezo na mapambo ya habari, au mambo yaliyo nyuma.

Contini-Morava ambaye amefanya uchambuzi wa ndani kuliko wengine kuhusu maana ya hali ya KI anasema kama muhtasari wa maoni yake:

> *ki* in fact means BACKGROUNDED, it is not just a "device" that happens to serve this discourse function. (1989:107f.)

Nimeshakubali kwamba hali ya KI inafaa sana kueleza mambo yaliyo nyuma ya habari kuu. Lakini bado nina wasiwasi fulani kusema kazi hii ya hali ya KI ni maana yake. Sababu zangu ni hizi zifuatazo.

Katika uchunguzi wake Contini-Morava analinganisha hali ya KI na hali za NA na KA. Mimi, katika muhadhara huu, nimelinganisha hali ya KI na maumbo ya vitenzi yenye kiambishi-rejeshi *-po-*. Ninavyoelewa, kazi ya kishazi-rejeshi ni kueleza na kupamba mambo mengine, yaani ni chombo cha kupanga sehemu ya habari iwe habari-saidizi, si habari kuu.

Tena, inaonekana kwamba lugha ya Kiswahili ina vyombo vingine vya kupanga utaratibu wa habari. Labda jukwaa la hadithi ni kubwa zaidi: mambo yanaweza kuwa mbele au nyuma au sehemu mbalimbali katikati. Tuangalie sentensi hizi:

(25) *Sudi hakukataa. Alikubali akasema, "Kweli, ni mimi niliye-mwandikia barua Bwana Kumba aipeleke kwa Mfalme."* (UK 25)
Sudi did not deny. He agreed AND SAID: "It is true, it is I who wrote this letter for Mr. Kumba so that he could send it to the King.

(26) *Wakati wote huo Sudi roho yake inamdundadunda, anasema, "Sasa ndiyo nimekwishajitia katika taabu, natafutwa na askari!"* (UK 25)
All this time Sudi's heart was beating fast, AND HE SAID: "Now I have really worked me into trouble, I am wanted by the police!"

(27) *Alibaki kubabaika tu na kusema, "Hawa jamaa nilikwisha zungumza nao na tukapatana nitawalipa."* (UK 3)
He was confused AND SAID: "These people, I had talked with them and we agreed I would pay them."

(28) *na kilu mtu alishika njia yake kwenda kumtafuta; kila mmoja akisema, "bila shaka nikimwona sitakosa kwa Mfalme."* (UK 44)
and everyone went his own way to look for her; everyone SAYING: "surely, if I find her I shall be rewarded by the king."


Katika sentensi hizi tunaona kitenzi *kusema* chenye hali mbalimbali, na umbo la *kusema* linafuatwa na maneno yanayotamkwa. Kila mara, kusema huko si hatua katika mstari wa hadithi lakini inatokea wakati ule ule kama tukio lililotajwa katika kishazi kitanguliacho. Bila shaka, kila umbo la kitenzi *kusema* lina maana yake na ujumbe wake wa pekee, ingawa tofauti hizo zisingeonekana tungepata hadithi hii katika sinema badala ya kuisoma kwenye kitabu. Ninayotaka kusema ni hayo: Lugha ya Kiswahili inatumia vyombo zaidi ya kimoja kupanga utaratibu wa lugha, na kwa hiyo, nina taabu kusema kwamba BACKGROUNDED ni maana halisi ya hali ya KI.

Zaidi ya hilo nina wasiwasi mwingine. Katika riwaya yetu tunakuta mifano mingi ya hali ya KI ambayo haipatani vizuri na maana ya kueleza habari-saidizi. Tazama mfano ufuatao:

(29) *Alilala chali akihesabu pau na huku akifikiria la kufanya.* (UK 9)
He lay on his back counting the beams and all this time thinking what to do.

Katika sentensi hii, habari kuu, yaani habari iliyo muhimu kwa maendeleo ya hadithi ni kwamba shujaa wetu anatafuta njia ya kujiepusha na shida zake. Habari kuu si kwamba amelala, kichali au kwa namna nyingine, hata si idadi ya pau darini. Vishazi vitatu vya sentensi hii vinapanga habari kwa viwango vitatu. Kiwango cha kwanza, kilicho ni karibu na msikilizaji au msomaji, kinatumia hali ya LI: *alilala chali*. Kwenye kiwango cha pili, mbali kidogo, kumepangwa kazi ya kiakili na kutumia hali ya KI: *akihesabu pau*. Lakini kuhesabu si makusudi ya mlalaji, anahesabu pau ili atulize fikra zake zinazomzungukia-zungukia kichwani. Kwa hiyo jambo la ndani kabisa limepangwa kwa kiwango cha tatu: *na huku akifikiria la kufanya*. Mwandishi ametumia hali ya KI pamoja na *huku;* kazi ya neno *huku* ni kueleza kwamba tumerukia kiwango kipya, bila ya ile *huku* tungefahamu kwamba bado tupo kwenye kiwango kile cha kuhesabu pau.

(30) Mpango wa sentensi [29] kwa viwango vitatu:




Kwa ajili ya mifano kama hii nafikiri kwamba maana halisi ya hali ya KI haihusiani na utaratibu wa usemi unavyofahamika kwa kawaida, yaani haitofautishi habari-saidizi na habari kuu. Bali, nadhani kwamba kazi yake inahusiana na kipengele kingine cha utaratibu wa habari: inaeleza hali ya ndani, na kinyume chake si lazima iwe habari kuu, lakini inaweza kuwa hali inavyoonekana usoni.

Hii inatusaidia kueleza jambo lingine: Tukiangalia orodha ya vitenzi vinavyotumika kwa hali ya KI ambavyo havielezi sharti, jumla yake katika riwaya yetu ni 34. Miongoni mwao, vitenzi 28 vinaeleza shughuli mbalimbali za kiakili au hali za kimoyo au maelezo ya nia au mambo mengine yasiyoonekani kwa macho, kama vile *kufikiri, kupenda, kuwa na hamu, kutazama, kutokuwa na akiba* n.k.

Basi, pendekezo langu kuhusu maana ya hali ya KI ni hilo:

| |
|---|
| Maana ya hali ya KI ni kueleza "hali ya ndani". Ikiwa inategemewa na kishazi cha kueleza tukio lisilotekelezwa huleta ujumbe kama sharti. Katika mazingira mengine inaleta ujumbe wa hali ilivyo, ambayo inaweza kuwa ni habari-saidizi, lakini mara nyingi ni habari kuu iliyofichwa nyuma ya matukio mengine yanavyoonekana usoni. |

## Marejeo

Ashton, E. O. 1944. *Swahili Grammar (including intonation).* London: Longmans.

Contini-Morava, Ellen. 1989. *Discourse Pragmatics and Semantic Categorization: The case of negation and tense-aspect with special reference to Swahili.* (Discourse Perspectives on Grammar, 1.) Berlin: Mouton de Gruyter.

Dammann, Ernst. 1956. Das situative Formans *ki* in einigen Bantusprachen. *Mitteilungen des Instituts für Orientforschung* 4:424-434.

Delius, Siegfried, and K. Roehl. 1939. [3rd ed.; 1st ed. 1910.] *Wegweiser in die Suaheli-Sprache.* Rügenwalde: Albert Mewes Nachf.

Kapinga, M. C. 1983. *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu.* Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Mfaume, Gideon Evans. 1984. *Misingi ya isimu ya lugha ya Kiswahili.* Dar es Salaam: Utamaduni Publishers.

Schadeberg, Thilo C. 1992. *A Sketch of Swahili Morphology.* Cologne: Rüdiger Köppe.

Schadeberg, Thilo C., and P. S. E. Elias. 1989. *AINI: A morphological parser for Kiswahili.* Leiden University.

Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. 1990. *Kamusi sanifu ya isimu na lugha.* Dar es Salaam: TUKI.

Wesana-Chomi, E. 1986. The status of *nga, nge* and *ki* in Kiswahili. *Kiswahili* 53,1/2:50–66.